Dawa dawaa

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza.

Waandishi:
Richard Mabala na Churchill Shakim

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Justice Rutenge na Evarist Kamwaga, Twaweza

Usanifu:
Churchill Shakim

©Tamasha/Twaweza - 2013

Barua:
TAMASHA
S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255-714-661-544
Baruapepe: vtamasha@gmail.com
general@tamashavijana.org
Wavuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili nakutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Wapendwa wasomaji,

Naomba niulize maswali kidogo:

Hali ya zahanati zetu na vituo vya afya ikoje?
Dawa zinatolewa palepale kituoni au tunaambiwa kwenda kununua?

- Tunauziwa dawa kwa bei ya chini kama ilivyoagizwa na Serikali, kwa mfano dawa ya mseto kwa ajili ya malaria au bei imepandishwa?
- Katika hali hiyo tunafanya nini? Tunamezea? Tunalalamika kichinichini? Au tunachukua hatua?
- Tusipochukua hatua, hali hii itaendelea hadi lini? Kulalamika bila kutenda ndio Utanzania kama wengine wanavyosema?

Haya. Pia kuna kamati maalum ya kutuwakilisha katika kusimamia haki zetu za afya.

- Tumehusika vipi katika kuchagua kamati hii?
- Tunawafuatilia kwa vipi?

Na mwisho, wakati tunalalamika sana kuhusu viongozi wabovu tusiowafahamu, tuko tayari kuwachukulia hatua wale ambao ni marafiki zetu au ndugu zetu? Kwa nini?

Hebu tuone wengine wanajibuje maswali hayo katika hadithi inayofuata.

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha.

Wahusika

Bonge
Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo
na mkereketwa wa maendeleo

Bibiye
Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Mwenyekiti
Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mtendaji
Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Bibi
Bibi yake Bibiye, anayewaunganisha wanawake ili kuchukua hatua za kuboresha hali ya jamii yake

Haya, una upungufu wa damu na malaria. Nunua dawa hizi.
Mbona anapaswa kupewa bure?
Hakuna dawa hapa. Itabidi kununua dukani.

Mmh! Nitapata wapi pesa zote hizo? Basi nipe za malaria tu.
Shilingi elfu tatu.
Mbona inapasua kuwa elfu moja tu.
Hapa si Ustawi. Tunafanya biashara.

Haiwezekani. Tunajua michezo yenu michafu.
Shikamoo bibi.
Marahaba.
Shoga!

Huyu ndiye rafiki yako? Mmmh!
Kuna nini shoga?
Ah hawa watu mabahili kama nini? Wanataka dezo kila kitu.

Lakini biashara nzuri. Mambo mazuri hapa.
Si wewe unajua dada, hospitali hakuna dawa.
Kwani ninyi mnapata wapi?

Kwani hujui? Kuvuja kwa pakacha.
Lakini wagonjwa wanateseka.
Shauri yao. Unataka nimwage unga?

Wanishangaza mwanangu. Nilikuheshimu sana maana unaelimisha vizuri. Lakini kwanini unaendekeza maovu?
Njoo haraka. Amezimia. Na damu inatoka.
Hebu tumuite Mawazo amkimbize hospitali.

Mimi siwaelewi. Ninawaandikia dawa lakini hamtaki kununua. sasa angalia.
Lakini dawa ni bei mbaya.
Kwani kosa langu? Hawaleti dawa za kutosha hapa. Zikiisha nifanye niini?

Si umsaidie basi.
Hivi hivi tu wakati amejitakia mwenyewe. Hapo lazima tusaidiane.


Huyu daktari amezidi. Anacheza na roho za watu.
Mwenye uroho anajali roho za wengine?
Hata huu uhaba wa dawa nina wasiwasi...


Mwenzenu ana hali mbaya sana. Itabidi apelekwe hospitali ya wilaya.
Tutapata wapi pesa?
Changamkeni. Mkizubaa shauri yenu.


Mawazo akichangisha fedha na kumkimbiza hospitali

Nawashukuru sana vijana. Mjukuu wangu amepata nafuu. Nusura apoteze mtoto.
Loh! Pole mama.
Lakini mbona nyie vijana mnakaa mnaangalia tu. Hata sisi wazee hatupati haki zetu.

Amesema kweli. Tukae tu tukiangalia hadi lini?
Yule daktari anapeleka dawa zetu kule dukani.
Kweli. Yeye na mwenzie wote waadabishwe.

Lakini tuwe makini jamani. Watu watamwaga unga.
Unaona! Mwelimishaji rika gani wewe?
Unatetea unga wa shoga badala ya afya ya wote? Wako wangapi wanaoumwa kwa sababu yao?

Wanamwendea mjumbe wa kamati ya afya
Nifanye nini miye? Wenzangu wote wamepachikwa na daktari mwenyewe...
Huo si utaratibu. Kamati imekamatika.
Kweli. Zikija dawa anawaita wale watu wake. Kisha unaona dawa zimehamia dukani.

Kwa nini hujachukua hatua? Ungetoa taarifa.
We bwana unathamini usalama wangu kweli?
Nathamini usalama wa wananchi wanaokosa dawa. Twende kwa mwenyekiti.

Ofisini kwa Mwenyekiti
Ohoo, Wakorofi wangu wameingia. Kuna nini leo?
Hali ya dawa ni mbaya. Daktari anatoa kwa mwenye duka na huyo mwenye duka anaziuza kiholela.

Ngoja kwanza. Una ushahidi wa kutosha?
Twende dukani na kufanya msako.
Chondechonde. Huyu si alitoa ardhi kwa ajili ya kituo cha polisi! Watu wataelewa tukimkamata?

Njoo haraka mwenyekiti. Kuna fujo pale kwenye duka la dawa.
Haya sasa. Wameshaelewa!

Mjukuu wangu kidogo afe na bei zenu.
Dawa zenu zinatoka wapi?
Iweje zahanati dawa hazikai wakati dukani kwako hazikauki?
Tokeni huko. Tokeni.

Jamani tumesikia kilio chenu. Hawa vijana walileta malalamiko kwangu. Mgambo tuanze uchunguzi.
Na wewe! Sikutegemea

Haya wananchi. Hawa watu mnawaona? Kwanza kamati ya afya imejiuzulu.
Safiii!
Na daktari na mwenye duka wamekiri makosa yao. Na tumewapa onyo kali na kutoa taarifa wilayani.

Haitoshi. Wafukuzwe kabisa Hatuwataki.
Tutapata wapi wengine wa kuchukua nafasi yao? Tuwaache lakini wakirudia yale yale tunawapeleka mbele ya sheria.
Na warudishe pesa za hongo, zitumike kuwanunulia wazee dawa zao.

Lakini jamani shoga, mbona mmetuumbua hivi?
Wewe ulinidanganya shoga, na kuwasingizia watu ili kuficha udhalimu wenu.
Kweli kabisa. Aheri kuumbua kuliko kuua.

Je wajua?

Kamati ya zahanati/kituo cha afya ni muhimu sana, maana, kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali, ina kazi ya kuangalia:

a. Usimamizi wa fedha. Hii ni pamoja na kuhakikisha usalama wa fedha zilizokusanywa.

b. Usimamizi wa wafanyakazi, na kushauri
Halmashauri kuhusu maendeleo ya watumishi katika nyanja za ajira, mafunzo, mgawanyo, maendeleo na motisha.

c. Usimamizi wa vifaa na majengo.

Tufanyeje?

- Kujua muundo wa kamati ya afya na kutumia nafasi ya uchaguzi kuwachagua wajumbe wanaofaa.
- Kusaidia kamati kuhakikisha kwamba dawa inatolewa ipasavyo
- Kutoa taarifa ya kudaiwa rushwa badala ya kutoa rushwa.
- Kuhakikisha kwamba wanawake wajawazito, watoto wadogo na wazee wasio na uwezo wanapata haki yao ya matibabu na dawa bure bila wasiwasi.
- Kuhakikisha kwamba sisi wenyewe, na watu wote wanapata na kumaliza dozi kamili ya dawa.

Je, umewahi kufanya jambo lolote la kishujaa kama Bonge na Bibie?

Au unamfahamu mtu mwingine aliyefanya kitu cha kipekee kuisaidia jamii yake?

Kama jibu ni ndiyo, tungependa utusimulie!

Tafadhali tutumie hiyo stori yako iliyoleta mabadiliko hapo unapoishi au iliyotokea mahali pengine.

Tunaweza kuitumia stori yako kuandaa vijitabu au vipindi vya Televisheni na redio ili kuelimisha wengine. Usikose kutumia fursa hii!

Anuani:
Barua: Twaweza-Shujaa, S.L.P 38342, Dar es Salaam
Barua-pepe: shujaa@twaweza.org
Simu: Tuma ujumbe mfupi (SMS) bure ukijumuisha neno SHUJAA kwenda **namba 15381**